

HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO

SIMU NA: 027 - 2552000
MOB NA: 0677 - 010213
FAX NA: 027 - 2552020
Email: ded@kitetodc.go.tz
info@kitetodc.go.tz



OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),
S.L.P. 98,
KIBAYA - KITETO

Kumb. Na. HMW/KTV/21/VOL.I/94

14 Julai, 2021

Yah: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO ANAWATANGAZIA
WANANCHI WOTE WENYE SIFA KUOMBA NAFASI YA KAZI IFUATAYO:

1. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III (NAFASI 1)

SIFA ZA MWOMBALI:

- Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) au sita (Form VI)
- Awe amehitimu Mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani za Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU:

- (i) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao.
- (ii) Kuratibu na kusimamia Upangaji na utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya Kijiji
- (iii) Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- (iv) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- (v) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na taratibu za Serikali.
- (vi) Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- (vii) Kuandaa taarifa za utekelezaji wakazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza shughuli za uzalishaji mali.

MSAHARA:

Ngazi ya Mshahara wa Serikalini **TGS B** kwa mwezi.

MAELEZO YA JUMLA NA UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI:

1. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenyewe umri usiozidi miaka 45.
2. Waombaji wote waambatanishe na nakala za vyeti vya elimu, taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha ndogo mbili za rangi (passport size).
3. Waombaji wote waaambatanishe na maelezo binafsi yaliyojitosheleza na yawe na anuani na namba ya simu.
4. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza na Mamlaka husika (TCU na NECTA).
5. Waombaji watakaoitwa kwenye usaili watatakiwa waje na vyeti halisi (Original Certificates).
6. Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto,
S.L.P 98,
KIBAYA – KITETO.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30/07/2021 saa 9:30 Alasiri.



Tamim H. Kambona
Mkurugenzi Mtendaji (W)
KITETO